



Haki na hali za ajira



Ni nini wewe unachofaa kutarajia katika kazi



Wakati unapoipata kazi na unapoenda kazini nchi Australia wewe unazo haki.



Haki zako huhakikisha kuwa wewe unapata:


- kulipwa mshahara sawa kwa kazi unayoifanya wewe



- kulipwa kwa masaa sawa uliyoyafanyia kazi wewe



- posho za kulipwa au pesa za ziada unazostahili wewe kama vile



- muda wa ziada kwa kufanya saa zaidi kuliko kawaida
- viwango vya adhabu – kiwango cha juu cha kulipa kwa kufanya kazi wikendi au sikukuu za umma



- likizo ya ugonjwa ikiwa unaihitaji



- mahali penye usalama pa kufanyia kazi



Pia una haki ya kujiunga na chama cha wafanyakazi.



Chama cha wafanyakazi ni shirika linalotunza watu wanaofanya kazi katika kazi za aina sawa.



Kuna watu ambao wanaweza kukusaidia kujua haki zako ni nini:

- mwajiri wako



- mpendekezo wako



- mfanyakazi wa kesi yako



Wewe unaweza kuwa na haki tofauti kulingana na hali unayoishi.

Hali ya kikazi



Kazi inaweza kuwa na hali nyingi tofauti.

Ikiwa kazi yako sio ya kudumu wewe unalipwa malipo zaidi kama vile:

- likizo ya ugonjwa
- likizo ya kulipwa


Marahehe		
9:00am	5:00pm	= \$\$\$
9:00am	5:00pm	= \$\$\$
9:00am	1:00pm	= \$\$

Ikiwa kazi yako ni ya muda mfupi utapata kulipwa masaa uliyofanyia kazi tu.



Wewe unaweza kufanya kazi:

- kazi yenye kuchukua muda wako kamili – kila siku



- kazi inayokuchukua sehemu ya muda wako – siku kadhaa

9:00am – 5:00pm



- wakati wa masaa ya biashara – saa 3 asubuhi hadi saa 11 jioni



- usiku



Wewe unapaswa tu kuchukua kazi ikiwa unaweza kufanya kazi masaa unayohitajika.



Mambo mengine muhimu yanaweza kuathiri masaa unayoweza kufanya kazi:

- jamii




- ahadi za kielimu
 - mafunzo unayohitaji kufanya
 - masomo unayohitaji kusoma



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kwenye tovuti ya Usawa Kazini (Fairwork).

www.fairwork.gov.au


Pesa zinazotolewa kutoka mshahara wako



Wakati mwingine pesa hutolewa kutoka mshahara wako kwa kulipia vitu vya muhimu.

Hizi zinaitwamatumizi kuondolewa au punguzo.

Matumizi kuondolewa yanaweza kufanywa kwa:



- ushuru – pesa unahitaji kulipa Serikali



- ada ya chama ikiwa wewe ni mwanachama wa chama



- manufaa mengineo



Waulize watu unaowajitahidi kukuambia kuhusu punguzo zako wakati unapoanza kazi yako.

\$\$\$

Bili



\$\$\$

Kodi



Unaweza pia kuchagua kuwa na fedha zichukuliwe ili kulipa bili au kodi.

Bima ya malipo ya uzeeni



Malipo ya Uzeeni ni njia mojawapo ya kuokoa pesa ili kuzitumia kuishi wakati unapostaafu kikazi.




Ni kawaida kwa watu kuacha kufanya kazi – kustaafu – wakati wa umri wa miaka 65.



Karibu kila mtu ambaye ana kazi lazima ajiunge na mfuko wa malipo ya uzeeni.

Chini ya sheria, watu unaofanya kazi kwa ajili yao walipe pesa katika mfuko wako wa nyongeza.



Unaweza pia kuweka pesa za ziada katika mfuko wako wa nyongeza ukitaka.



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi juu ya malipo ya uzeeni kwenye Ofisi ya Ushuru wa Australia (Australian Taxation Office - ATO) pamoja na tovuti za Utumaiji wa Fedha Vizuri (Moneysmart).

- www.ato.gov.au/super/
- www.moneysmart.gov.au/superannuation-and-retirement

Afya na usalaam kazini



Kila jimbo na wilaya ina sheria zinazosaidia watu kuwa salama wakati wa kazi.

Sheria hizi zikiwemo:



- kukupa wewe nafasi yenye usalama ya kufanyia kazi ambayo ina msaada unaoweza kuitumia ikiwa unaihitaji




- kukufundisha kuhusu mambo yasiyo salama



- kuhakikisha kuwa una afya wakati unafanya kazi



- kuwa na wafanyakazi ambao wanajua mengi kuhusu afya na usalama na wanaweza kusaidia wengine



Wewe unahitaji kufuata sheria zinazohusu afya na usalama katika mahali pa kazi yako.

Wewe unafaa:



- kufanya yale mameneja wako wanayokuomba wewe kufanya



- kuvaa mavazi ambayo yanakuhifadhi kwa usalama



- hakikisha matendo yako hayawezi kukuumiza wewe au watu wengine



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kwenye tovuti ya Usalama Kazini (Safework).

www.safeworkaustralia.gov.au

Ukurasa huu umewachwa tupu makusudi



Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji
la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya
Huduma za Jamii nchini Australia

